# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.18 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) AGOSTI 2022


# TSC KUTUMIA MFUMO WA KIELEKTRONIKI (TSCMIS) KUHUDUMIA WALIMU



*Timu ya Wataalamu wa ujenzi wa Mfumo wa Kielektoniki wa TSC (TSCMIS) wakifuatilia kwa makini wasilisho la vipengele vya mfumo huo linalofanywa na wataalamu wenzao (hawapo pichani) hivi karibuni mkoani Morogoro.*


**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

# HONGERA TSC KWA KUENDELEA KUBORESHA UTOAJI WA HUDUMA KWA WALIMU

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imejipanga kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki unaojulikana kama "Teachers Service Commission Management Information System" (TSCMIS) katika kutoa huduma zake kwa walimu. Mfumo huu unakuja kutatua changamoto za utoaji huduma zilizokuwa zinawaathiri wateja (walimu na wadau wengine).

Tunaipongeza Menejimenti ya TSC inayoongozwa na Mwl. Paulina Nkwama kwa kuamua kutafuta ufumbuzi utakaoweza kurahisisha utendaji kazi pamoja na kumwondolea mwalimu usumbufu wa kutembembea kwenye ofisi za TSC kuulizia maendeleo ya hoja au majibu ya masuala yake aliyoyawasilisha.

Mfumo huu ni wa muhimu kwa kuwa utamsaidia mwalimu hata akiwa nyumbani kwake kuweza kujua suala lake aliloliwasilisha TSC limefikia wapi kwani ataweza kwa kuingia kwenye mfumo huo na kupata taarifa anazohitaji kwa kutumia hata simu yake ya mkononi ikiwa na mtandao wa intaneti.

Mfumo huu pia utasaidia kutunza kumbukumbu, nyaraka na vielelezo mbalimbali hususani katika masuala ya mashauri ya nidhamu kitu ambacho kitasaidia uendeshaji wa mashauri na rufaa kufanyika kwa ufanisi zaidi na hivyo kutoa haki kwa wakati.

Zipo faida nyingi za mfumo huu ambazo hatuwezi kuzielezea hapa lakini matarajio yetu ni kwamba mfumo huu umekuja kuleta mageuzi makubwa ya utendaji wa kazi za TSC, hivyo walimu watarajie kupata huduma bora zaidi kuliko wanavyohudumiwa sasa.

Tunaamini kwamba watumishi wa TSC pamoja na wadau wengine wanaohusika kuutumia mfumo huu watafanya kazi zao kwa weledi, ubunifu na maarifa zaidi ili kuhakikisha thamani ya fedha zilizowekezwa na Serikali katika kuujenga mfumo huo zinaleta tija katika kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa walimu na wadau wengine.


## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina Nkwama

**Wajumbe**
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya
Zachary A. Dida

**Mhariri Mkuu**
Gerard Chami

**Mhariri**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon


## KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

# TSC KUTUMIA MFUMO WA KIELEKTRONIKI (TSCMIS) KUHUDUMIA WALIMU

**Na Mwandishi wetu – Morogoro.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ipo mbioni kukamilisha ujenzi wa Mfumo wa kielektroniki unaojulikana kama "Teachers Service Commission Management Information System" (TSCMIS) kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi wa kila siku pamoja na kuwahudumia walimu kwa urahisi na haraka zaidi katika masuala ya ajira, rufaa, nidhamu na maendeleo yao.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni katika taarifa iliyohusu hatua ya utekelezaji wa mfumo wa TSCMIS ambayo ilieleza kuwa Mfumo huo ambao utafanya kazi kuanzia ngazi ya Shule, TSC Wilaya hadi TSC Makao Makuu unajumuisha moduli saba ambapo katika awamu ya kwanza ya ujenzi wa mfumo huo moduli tatu zinatarajiwa kukamilika hivi karibuni na zitafanyiwa majaribio katika Mikoa minne ya Dar es Salaam, Dodoma, Iringa na Mwanza kuanzia mwezi Septemba 2022.

"Moduli tatu zinazotarajiwa kukamilika hivi karibuni ni zile zinazohusika na Appeal (Rufaa), Disciplinary (Mashauri ya Nidhamu) na Compains (Malalamiko) huku moduli nyingine 4 za "Appointment and Development" (Ajira na Maendeleo), "Visitors" (wageni), "Helpdesk" & "Gratuity Computation" (Dawati la Msaada na Ukokotoaji wa Mafao) zimepangwa kuendelea kujengwa katika awamu ya pili ya ujenzi wa Mfumo huo," ilieleza sehemu ya Taarifa hiyo.

Taarifa ilisisitiza kuwa ujenzi wa Mfumo wa TSCMIS umezingatia mwongozo uliotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) na kufuata hatua mbalimbali katika ujenzi wake ikijumuisha kubainisha mahitaji, kusanifu na kujenga Mfumo, majaribio, kusimika na kusimamia Mfumo pamoja na mafunzo kwa watumiaji.

Mfumo wa TSCMIS unarajiwa kuwa na faida kwa Tume na wadau mbalimbali kwa kuwa utarahisisha mchakato kushughulikia mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kuanzia ngazi ya shule, Ofisi za Wilaya hadi Makao Makuu; utasimamia na kufanya ufuatiliaji wa hatua za mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu; utapunguza makosa, gharama na muda huku ukiongeza ufanisi wa kushughulikia mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu.



*Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Takwimu wa TSC, Kainda Ndasa akikagua kazi inayoendelea ya ujenzi wa mfumo wa kielektroniki wa Tume (TSCMIS) inayoendelea kufanywa na wataalamu kutoka TSC na Taasisi nyingine za Serikali mjini Morogoro.*



*Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Takwimu wa TSC, Kainda Ndasa akikagua kazi inayoendelea ya ujenzi wa mfumo wa kielektroniki wa Tume (TSCMIS) inayoendelea kufanywa na wataalamu kutoka TSC na Taasisi nyingine za Serikali mjini Morogoro.*

# TSC KUTUMIA MFUMO WA KIELEKTRONIKI (TSCMIS) KUHUDUMIA WALIMU

Faida nyingine za mfumo huo ni kurahisisha mchakato wa kuwasilisha viambatisho mbalimbali vinavayohusu masuala ya Mashuari ya Nidhamu, Rufaa Malalamiko, Mafao na Mirathi; Mfumo utarahisisha zoezi la kutoa namba za usajili za walimu (TSC Number); Mfumo utakuwa na uwezo wa kutoa taarifa (notification) zilizopokelewa na kuwasilishwa kuhusu masuala ya Mashauri ya Nidhamu, Rufaa, Malalamiko, Mafao na Mirathi; mfumo huo pia utakuwa na uwezo wa kutoa mrejesho (feedback) kuhusu malalamiko yaliyowasilishwa.

"Pamoja na hayo, mfumo huo utapunguza matumizi ya karatasi na kuboresha utunzaji na upatikanaji wa taarifa; Mfumo huo utarahisisha upatikanaji wa ripoti mbalimbali kwa wakati; utarahisisha mawasiliano na utendaji kazi katika Ofisi za Tume kuanzia ngazi ya Wilaya, Makao Makuu na Wadau mbalimbali na kusimamia na kutunza rekodi za wageni wanaofika TSC kwa lengo la kupata huduma," ilisema taarifa huyo.


Taarifa hiyo ilifafanua kuwa kwa sasa Mfumo upo kwenye hatua ya kufanyiwa majaribio




*Wataalamu wanaojenga Mfumo wa Kielektroniki wa TSC (TSCMIS) wakijadiliana jambo ikiwa ni sehemu ya kazi ya ujenzi wa mfumo huo inayofanyika mkoani Morogoro.*

na watumiaji (User Acceptance Test - U.A. T) ili kujiridhisha na utendaji kazi wake katika moduli tatu (Appeal, Disciplinary na Complaints) zilizokamilika, hatua ambayo inakwenda sambamba na kufanya maboresho (bug fixing) ili kuuweka sawa na tayari kwa kuanza kutumika kwenye Mikoa ya majaribio.

Ujio wa mfumo huo ni mwarobaini wa changamoto mbalimbali zilizokuwa zinaikabili TSC zikiwemo kutokuwa na taarifa/rekodi sahihi (unreliable data), kushindwa kushughulikia masuala ya rufaa, nidhamu na malalamiko ya walimu kwa ufanisi pamoja na kutumia muda mrefu, gharama kubwa katika utekelezaji wa shughuli za kila siku.



*Wataalamu wanaojenga Mfumo wa Kielektroniki wa TSC (TSCMIS) wakiendelea na kazi mkoani Morogoro.*



*Mmoja wa wataalamu wanaojenga Mfumo wa Kielektroniki wa TSC (TSCMIS) akiendelea na kazi ya kujenga mfumo huo mkoani Morogoro.*

# TSC KUTUMIA MFUMO WA KIELEKTRONIKI (TSCMIS) KUHUDUMIA WALIMU








*Wataalamu wanaojenga Mfumo wa Kielektroniki wa TSC (TSCMIS) wakiendelea na kazi mkoani Morogoro.*



*Baadhi ya wataalamu wanaojenga mfumo wa Kielektroniki wa TSC (TSCMIS) wakifanya wasilisho kwa wenzao juu ya vipengele vinavyotakiwa kuwepo kwenye mfumo huo.*



*Sehemu ya mwonekano wa mfumo w a kielektroniki wa TSC (TSCMIS) unaoendelea kujengwa.*



*Timu ya Wataalamu wa ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa TSC (TSCMIS) wakifuatilia kwa makini wasilisho la vipengele vya mfumo huo linalofanywa na wataalamu wenzao (hawapo pichani) hivi karibuni mkoani Morogoro.*

# TUMEENDELEA KUWAELIMISHA WATUMISHI WETU PAMOJA NA WALIMU KUJIEPUSHA NA RUSHWA: NKWAMA

**Na Mwandishi wetu – Dodoma.**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Kuzuia Rushwa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Sabina Seja juu ya masuala mbalimbali yanayohusu utumishi wa walimu na namna ya kuzuia rushwa.

Mazungungumzo hayo yalifanyika hivi karibuni katika Ofisi ya TSC Makao Makuu Dodoma ambapo Katibu wa Tume alimweleza Mkurugenzi huyo kuwa TSC imeendelea kutekeleza majukumu ya kuwahudumia walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016.



*Mkurugenzi wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupapana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Sabina Seja akisaini kitabu cha wageni wakati alipomtembelea Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (hayupo pichani) ofisini kwake TSC Makao Makuu Dodoma hivi karibuni.*

Nkwama alifafanua kuwa TSC inahusika moja kwa moja na maisha ya mwalimu tangu anapoajiriwa hadi anapostaafu, hivyo endapo watumishi wake hawatafanya kazi kwa uadilifu inaweza kuchochea rushwa na kusababisha chombo hicho kutofikia malengo yake ya kutoa huduma bora kwa walimu.

"TSC inahusika na kumsajili mwalimu katika



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akimwelezea Mkurugenzi wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa kutoka Taasisi ya Kuzuiana Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Sabina Seja nanma TSC inavyotoa huduma kwa walimu kwa mujibu wa sheria.*



*Mkurugenzi wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Sabina Seja (kulia) akimweleza Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama mbinu mbalimbali wanazotumia kukabiliana na rushwa katika jamii.*

# TUMEENDELEA KUWAELIMISHA WATUMISHI WETU PAMOJA NA WALIMU KUJIEPUSHA NA RUSHWA: NKWAMA

ajira, kumthibitisha kazini, kumbadilishia kazi au cheo mwalimu aliyejiendeleza kielimu, kumpandisha cheo mwalimu, kusimamia programu ya mafunzo kazini, kutoa vibali vya kustaafu kazi ya ualimu na kusimamia nidhamu na maadili ya walimu. Hivyo unaweza kuona kuwa kila jukumu linahusu maslahi ya mwalimu, hivyo tusipokuwa waadilifu ni rahisi sana rushwa kukithiri katika ofisi yetu na kutotenda haki kwa walimu", alisema Nkwama.

Kutokana na unyeti wa huduma zinazotolewa na Tume hiyo, Nkwama alieleza kuwa TSC imekuwa ikiwaelimisha watumishi wake juu ya umuhimu wa kuzingatia Miiko na Maadili ya Utumishi wa Umma katika kutoa huduma, na wakati wote kuhakikisha wanatenda haki kwa mujibu wa sheria.

Pamoja na hilo, Nkwama ameeleza kuwa wamekuwa wakifanya vikao mara kwa mara na walimu ambapo pamoja na kuwaelimisha haki na wajibu wao, wamekuwa wakiwakumbusha kuwa TSC inatoa huduma zake bure kwa mjibu wa sheria, hivyo wajiepushe na vitendo vya rushwa kwa kuwa vitendo hivyo sio kwamba ni kinyume na maadili ya utumishi wa walimu tu lakini pia vinasababishwa kukiukwa kwa haki katika kutoa huduma.

"Temeendelea kuwakumbusha watumishi wetu kuzingatia maadili ya kazi na wasijiingize kushawishi kupewa au kukubali kupokea rushwa kutoka kwa wateja. Kwa kweli tunaendelea kutoa huduma vizuri na malalamiko ya walimu yanaendelea kupungua. Lakini hatujaishia kwa watumishi wetu tu, mara kwa mara tunapofanya mikutano na walimu tumekuwa tukisisitiza kuepukana na vitendo hivyo pia," alisema Nkwama.

Nkwama alimweleza Mkurugenzi huyo kuwa TSC itaendelea kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na TAKUKURU ili kuhakikisha kuwa inazuia vitendo vyote vya rushwa kwa watumishi wa TSC na walimu na pale vitendo hivyo vinapotokea sheria ichukue mkondo wake mara moja ili kuleta ustawi mzuri kwa walimu.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akimwonesha Mkurugenzi wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Sabina Seja kitabu chenye Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448, Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016, Kanuni za Maadili ya Kazi ya Ualimu pamoja na Mwongozo wa Hatua za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akimwonesha Mkurugenzi wa Kuzuia Rushwa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Sabina Seja kitabu cha Taarifa ya Utafiti kuhusu Tathimini ya Utekelezaji wa Majukumu ya TSC tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016.*

# TUMEENDELEA KUWAELIMISHA WATUMISHI WETU PAMOJA NA WALIMU KUJIEPUSHA NA RUSHWA: NKWAMA

Naye Mkurugenzi wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa kutoka TAKUKURU, Sabina Seja alimpongeza Katibu wa TSC kwa jitihada nazofanya katika kusimamila Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu nchini huku akisisitiza kuwa jitihada za kuzuia rushwa zinapaswa kuwa endelevu ili kila mtumishi wa TSC na walimu kwa ujumla wasijiingize katika vitendo hivyo.

Alieleza kuwa Idara yake imejikita katika kuzuia rushwa kwa kutoa elimu kwa wananchi ili wajiepushe na rushwa wakati wote, hata hivyo alieleza kuwa pale ambapo watu wanaelemishwa lakini hawabadiliki ndipo inapowalazimu kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

"Kwetu elimu ni kipaumbele cha kwanza, ni wajibu wetu kutoa elimu kwa wadau wetu kabla ya kuanza kuchukua hatua. Tumepata mafanikio sana kwa kutoa elimu kwa wananchi na kwa kweli wengi wanabadilika na pale wanapoona kuna dalili za rushwa wanatupatia taarifa na sisi tunachukua hatua mara moja," alisema Mkurugenzi huyo.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akimwonesha Mkurugenzi wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Sabina Seja vipeperushi vya Ijue Tume ya Utumishi wa Walimu na Nguzo Kuu ya Maadili na Miiko ya Kazi ya Ualimu.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akimkabidhi Mkurugenzi wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Sabina Seja zawadi za vitabu na vipeperushi vya TSC wakati Mkurugenzi huyo alipotembelea ofisi za TSC Makao Makuu hivi karibuni.*

Katibu wa TSC alimpatia Mkurugenzi huyo kitabu chenye Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448, Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016, Kanuni za Maadili ya Kazi ya Ualimu pamoja na Mwongozo wa Hatua za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu.

Nkwama alimpatia Mkurugenzi huyo ni, Taarifa ya Utafiti kuhusu Tathimini ya Utekelezaji wa Majukumu ya TSC tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016, vipeperushi vya Ijue Tume ya Utumishi wa Walimu na Nguzo Kuu za Maadili na Miiko ya Kazi ya Ualimu.

# NYUMBA YA WALIMU, LUMUMA SEKONDARI KUJENGWA



*Waziri wa Nchi Ofisi ya waziri Mkuu sera Bunge na Uratibu (Mb) Mhe. George Simbachawene akizungumza na wananchi wa Lumuma katika Mkutano wa hadhara jimbo la Kibakwe Halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa.*

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Serikali kupitia Ofisi ya Rais Tamisemi imeahidi kujenga Nyumba ya walimu moja two in one itakayojengwa kwa kupitia mradi wa EP4R katika shule ya sekondari Lumuma iliyojengwa madarasa sita kwa nguvu za wananchi.

Hayo yamesemwa na Mbunge wa jimbo la kibakwe Halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa Mhe. George Simbachawene alipokuwa akihutubia mkutano wa hadhara, wananchi wa kata Lumuma baada ya kujionea maendeleo ya ujenzi wa shule hiyo.`

"gharama za matofali katika ujenzi wa nyumba hiyo ya walimu zitatolewa na nguvu kazi ya wananchi, na tunaweza kujenga nyumba mbili za aina hiyo kama tutakaza msuli vizuri alisema waziri"

Kupitia fedha za mfuko wa jimbo nitasaidia katika kukamilisha ujenzi wa miundo mbinu mingine, ikiwa ni pamoja na kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala.

Katika hatua nyingine Mhe. Waziri ameelekeza Halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa kusajili barabara ambazo hazijasajiliwa hasa zinazoenda kwenye maeneo ya huduma za kijamii au maeneo mapya ya utawala ambayo yameongezeka.

Halmashauri inapaswa kuzifungua na kisha kuzisajili kwa mujibu wa mchakato wa kisheria, ambapo lazima kamati ya maendeleo ya kata ikae na kuzibainisha baraba mahali zilipo na urefu wake na kuonesha taasisi inayokwenda ili kupeleka mapendekezo kwenye Halmashauri na baadae kupeleka



*Waziri wa Nchi Ofisi ya waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu (Mb) Mhe. George Simbachawene akikagua ujenzi wa shimo la choo katika sekondari ya Lumuma jimbo la Kibakwe Halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa.*

# NYUMBA YA WALIMU, LUMUMA SEKONDARI KUJENGWA



*Waziri wa Nchi Ofisi ya waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu (Mb) Mhe. George Simbachawene akikagua ujenzi wa shimo la choo katika sekondari ya Lumuma jimbo la Kibakwe Halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa.*

DCC na baadae kwenye bodi ya barabara ya mkoa ( Road Board).

"Barabara hizi zikisajiliwa kwa mujibu wa sheria ni rahisi kwa wakala wa barabara vijijini (TARURA) kuzitambua na kuzitengea fedha alisema Waziri"

Awali katika taarifa yake Diwani wa kata ya Lumuma Mhe. Joktan Chelligah amesema wananchi wa kata ya Lumuma wamejenga shule hiyo katika kipindi cha mwaka mmoja.

"Wananchi tumechanga fedha kiasi cha million 17, lakini Halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa imetuchangia million 20, na mifuko 150 ya saruji pamoja na mabati 250, na chama cha mapinduzi Mkoa wa Dodoma kimechangia mifuko 130 alisema"



*Waziri wa Nchi Ofisi ya waziri Mkuu sera Bunge na Uratibu (Mb) Mhe. George akikagua ujenzi wa miundo mbinu ya madarasa katika shule ya sekondari Lumuma jimbo la Kibakwe Halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa.*

# TSC YATIKISWA TENA, NI PAUL SALAMA LEKULE



*Jeneza lenye mwili wa aliyekuwa mtumishi wa TSC, Marehemu Paul Salama Lekule wakati wa Msiba uliofanyika wilayani Kongwa mkoani Dodoma hivi karibuni.*

**Na Mwandishi wetu - Dodoma**

Kwa mara nyingine tena Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imepata pigo baada ya kuondokewa na mtumishi wa wake, ndugu Paul Salama Lekule aliyekuwa Afisa Ajira katika ofisi ya TSC Wilaya ya Kongwa.

Mtumimishi huyo alifariki dunia tarehe 12 Julai, 2022 saa 7:38 mchana akiwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma alipokuwa akipatiwa matibabu ya kufuatia ugonjwa wa homa ya mapafu ambao ulikuwa ukimsumbua kwa muda mrefu.

Akizungumza wakati wa mazishi ya mtumishi huto yaliyofanyika Julai 16, 2022 wilayani Kongwa, Katibu wa TSC Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa ofisi yake imepokea kwa masikitiko makubwa msiba huo ikizingatiwa kwamba katika kipindi cha muda mfupi TSC imepoteza watumishi kadhaa



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia) akiwa na viongozi wengine wa TSC kwenye msiba wa Mtumishi wa TSC Wilaya ya Kongwa, Paul Lekule. Msiba huo ulitokea hivi karibuni na mazishi yalifanyikia wilayani Kongwa.*



*Baadhi ya Waombolezaji waliohudhuria msiba wa Mtumishi wa TSC Wilaya ya Kongwa, Paul Lekule uliotokea hivi karibuni katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma na mazishi kufanyika wilayani Kongwa.*

ambao wamefariki dunia kutokana na maradhi mbalimbali.

Alisema kuwa Marehemu Lekule ni mtu ambaye alikuwa mpole, mtaratibu huku akitekeleza majukumu yake kwa weledi na nidhamu jambo ambalo limekuwa moja ya sababu ya Ofisi ya TSC Wilaya ya Kongwa kuendelea kutoa huduma na kupunguza kero na malalamiko kwa walimu kwa kiasi kikubwa.

"Msiba huu umetugusa kipekee kwa kuwa marehemu Lekule alikuwa mtumishi mwezetu. Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu pamoja na Kamati ya Wilaya ya Tume ya Utumishi wa Walimu tunatoa pole nyingi kwa wote tulioguswa na msiba huu. Ninaomba pia mpokee salamu za pole kutoka kwa Makamishna wa TSC lakini pia salam za pole kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI)" alisema Nkwama wakati wa msiba huo.

Marehemu Paul Salama Lekule alizaliwa tarehe 28.07.1970 katika Kijiji cha Kiracha Wilaya ya Moshi Mkoa wa Kilimanjaro akiwa mtoto wa tatu wa Mzee Fabian Raura Lekule na Bi Grasiana Joseph Mberelie ambapo alipata elimu ya msingi katika Shule ya msingi Kiracha iliyopo Moshi Kilimanjaro mwaka 1990 na kuhitimu mwaka 1996.

Mwaka 1997 alijiunga na elimu ya Sekondari kidato cha kwanza, Shule ya Sekondari Hanga Moshi na kuhitimu kidato cha nne mwaka 2000, mwaka 2001 alijiunga na chuo cha Ualimu Bustani kilichopo Wilaya ya Kondoa Mkoa wa Dodoma na kutunukiwa Astashahada ya Ualimu IIIA mwaka 2004.

Mwaka 2009 alijiunga na Chuo cha ADEM kilichopo Wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani kusomea Stashahada ya Uongozi na Utawala katika Elimu na kutunukiwa Stashahada ya Uongozi na Utawala katika Elimu mwaka, 2011.

Kwa upande wa ajira, tarehe 07 Juni, 2004 Marehemu Lekule aliajiriwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa na kupangiwa Kituo cha kazi Shule ya Msingi Kibaigwa hadi mwaka 2008 alipopata uhamisho kwenda Shule ya Msingi Mlali "A" iliyopo Wilaya ya Kongwa.

Tarehe 01 Mei, 2013 Marehemu alipata uhamisho kwenda Tume ya Utumishi wa Umma, nakupangiwa kufanya kazi iliyokuwa Idara ya Utumishi wa Walimu na kupangiwa kufanya kazi katika Ofisi ya iliyokuwa Idara hiyo Wilaya ya Kongwa ambapo sasa ni Tume ya Utumishi wa Walimu, kama Afisa Ajira, Madaraja na Pensioni, cheo ambacho amedumu nacho hadi

# TSC YATIKISWA TENA, NI PAUL SALAMA LEKULE




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa heshima za mwisho wakati wa kuaga mwili wa aliyekuwa mtumishi wa TSC Wilaya ya Kongwa, Paul Lekule.*

# TSC YATIKISWA TENA, NI PAUL SALAMA LEKULE

umauti ulipomkuta.

Kwa mujibu wa wasifu wa Marehemu, tarehe 12 Juni, 2022 marehemu alianza kujisikia vibaya na kuamua kwenda Hospitali ya Wilaya ya Kongwa kwa matibabu. Kutokana na hali yake kuwa mbaya, alipewa rufaa kwenda Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Dodoma kwa matibabu zaidi, hadi umauti ulipomfika tarehe 12 Julai, 2022 saa. 7.38 Mchana.

Mbali na kuwa mtumishi wa TSC, Marehemu Paul Salama Lekule alikuwa mtumishi wa Mungu kupitia Shirika la Ndugu Wadogo Wafrasisko Wakapuchini lenye Makao Makuu yake nchini Itali, shirika ambalo linafanya utume wake chini ya misingi ya Kanisa Katoliki ambapo alijiunga na shirika hilo tarehe 04.08.1994 kama Mnovisi, na kuweka nadhiri za Daima tarehe 10.08.2003. Marehemu amefanya kazi ya utume akiwa katika Shirika hilo katika Parokia ya Kibaigwa, Mlali na Kongwa katika vipindi tofauti na hadi umauti wake alikuwa akifanya kazi ya utume Parokia ya Kongwa.



*Jeneza lenye mwili wa marehemu Paul Lekule likiwa kaburini tayari kwa ajili ya mazishi.*



*Baadhi ya Watawa wa Shirikala la Shirika la Ndugu Wadogo Wafrasisko Wakapuchini wakiaga mwili wa Mtawa mwezao ambaye pia alikuwa mtumishi wa TSC, Paul Lekule wilayani Kongwa hivi karibuni.*



# SHULE YA KATA MWANALUGALI YAANZA KWA KISHINDO UFAULU KIDATO CHA SITA

**Na Mwandishi wetu – Kibaha.**

Shule ya Sekondari Mwanalugali iliyopo Kata ya Tumbi katika Halmashauri ya Mji Kibaha imeanza vyema kwenye ufaulu wa matokeo ya Kidato cha Sita yaliyotangazwa Julai 5, 2022 kwa kufaulisha wanafunzi wote 32 sawa na 100 asilimia.

Mkuu wa shule hiyo Joseph Mkumbo amesema wanafunzi walianza masomo yao mwaka 2020 wakiwa ni chaguo la pili lakini kwa juhudi za walimu na wanafunzi wenyewe waliweza kupambana kimasomo na Sasa matunda yameonekana kwa ufaulu wa kishindo.

Mkumbo ameeleza kuwa kati ya wanafunzi 32, 23 wamepata daraja la pili na wanafunzi 9 wamepata daraja la tatu huku shule hiyo ikishika nafasi ya 27 kati ya shule 33 Kimkoa na Kitaifa ikishika nafasi ya 547 kati ya 644 kwa wastani wa G.P.A ya 3.1

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha Eng. Mshamu Munde ameipongeza

**“… kati ya wanafunzi 32, 23 wamepata daraja la pili na wanafunzi 9 wamepata daraja la tatu huku shule hiyo ikishika nafasi ya 27 kati ya shule 33 Kimkoa na Kitaifa ikishika nafasi ya 547 kati ya 644 kwa wastani wa G.P.A ya 3.1”.**

Idara ya Elimu Sekondari kwa usimamizi unaoleta tija kitaaluma.

Aidha, amewapongeza walimu, wazazi, jamii yote ya Mwanalugali na wanafunzi kwa jitihada zilizofanikisha matokeo hayo mazuri.

Marco Bahebe ambaye ni Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kibaha amewapongeza Walimu kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za kiutumishi na kusisitiza kwamba nidhamu ya walimu ndio chachu ya mafanikio ya shule hiyo.

Shule hii ilianza kudahili wanafunzi Mwaka 2020 kwa tahasusi ya HGL hivyo hayo ndiyo matokeo yake ya kwanza ya Kitaifa kwa Kidato cha Sita.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)

OFISI YA RAIS
Tume ya Utumishi wa Walimu
(TSC)



*Baadhi ya viongozi na maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa kwenye kikao cha kupitia miradi ya wafadhili wa TSC, kikao hicho kimefanyika hivi karibuni katika ukumbi wa mikutano wa TSC Makao Makuu jijini Dodoma.*



*Baadhi ya viongozi na maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa kwenye kikao cha kupitia maandiko ya miradi ya wafadhili, kikao hicho kimefanyika hivi karibuni katika ukumbi wa mikutano wa TSC Makao Makuu jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi wa Idara ya Utawali na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa TSC, Zachary Dida (kushoto) akiongoza kikao cha kupitia miradi ya wafadhili wa TSC. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Makao Makuu jijini Dodoma. Pembeni yake ni Afisa Tawala Mkuu wa TSC, Omar Ilyas.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mipango Ufuatiliaji na Tathmini, Evodia Pangani (kushoto) wa TSC akitoa maelezo juu ya miradi ya wafadhili katika kikao kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma. Pembeni yake ni Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Hamari na Mawasiliano wa TSC, Kainda Ndasa.*



*Baadhi ya wajumbe wa Kikao cha kupitia miradi ya wafadhili wa TSC wakifuatilia kwa makini kinachoendelea katika kikao hicho kilichofanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma.*

# SHULE YA KATA ZOGOWALE YAENDELEA KUNG'ARA UFAULU KIDATO CHA SITA

**Na Mwandishi Wetu – Kibaha.**

Shule ya Kata Zogowale iliyopo Kata ya Misugusugu, Halmashauri ya Mji Kibaha imeendelea kung'ara kwenye ufaulu wa matokeo ya Kidato cha Sita mwaka 2022 yaliyotangazwa tarehe 5 Julai, 2022 kwa kufaulisha kwa 100 asilimia.

Mkuu wa shule hiyo Tatu Mwambala amesema kuwa ufaulu umekuwa wa kuridhisha zaidi Mwaka huu kwa kupanda kutoka GPA ya 3.4 Mwaka 2021 mpaka 3.2 Mwaka huu.

Mwambala amesema kuwa wanafunzi 7 wamepata daraja la kwanza, 87 daraja la Pili, 78 daraja la 3 huku wanafunzi 2 wakipata daraja la nne.

Mwambala ameongeza kuwa ingawa hakuna aliyepata daraja sifuri kati ya wanafunzi 174 lakini Kimkoa imekuwa nafasi ya 31 kati ya shule 45 huku Kitaifa ikishika nafasi ya 592.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha Mhandisi Mshamu Munde, ameipongeza Idara ya Elimu Sekondari kupitia kwa Mkuu wa Idara hiyo, Mwl. Rosemary Msasi kwa usimamizi Mzuri, Walimu, Wazazi na wanafunzi wenyewe kwa mafanikio hayo na kwamba hii iwe Chachu zaidi kwa miaka mingine.

Aidha, Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSSC) Wilaya ya Kibaha Marco Bahebe kando ya kuwapongeza amesema mafanikio haya yametokana na nidhamu na matumizi sahihi ya Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma.

Shule ya Sekondari Zogowale inafundisha tahasusi za HGK, HKL, CBG na PCB.

> **"... mafanikio haya yametokana na nidhamu na matumizi sahihi ya Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma.".**

# Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
# OFISI YA RAIS
# Tume ya Utumishi wa Walimu

## KAULI MBIU NANE NANE 2022:

***Ajenda 10/30: Kilimo ni Biashara, Shiriki Kuhesabiwa kwa Mipango Bora ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi"***

www.tsc.go.tz

## DIRA

"Kuwa Taasisi inayoongoza kwa kutoa huduma bora kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari waliopo kwenye Utumishi wa Umma."

## DHIMA

"Kutoa huduma bora kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari kupitia Ajira, Upandishwaji Vyeo na Kukuza Maadili."

"Mwalimu ni Chimbuko la Kada zote ndani na nje ya Utumishi wa Umma, hivyo anapaswa kuheshimi-wa, kujiheshimu na kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu."

**MAWASILIANO:**
Wasiliana na Katibu Msaidizi katika Wilaya yako au Tume Makao Makuu kupitia:-

KATIBU,
Ofisi ya Rais,
Tume ya Utumishi wa Walimu,
Mtaa wa Mtendeni,
S. L. P 353,
DODOMA - TANZANIA.

Simu: +255(26) 2322402-4
Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz
Tovuti: www.tsc.go.tz
Ukurasa wa FB: Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania,
Instagram: tumeyautumishiwawalimu
YouTube: TSC Digital Tv

DIRA

"Kuwa Taasisi inayoongoza kwa kutoa huduma bora kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari waliopo kwenye Utumishi wa Umma."

DHIMA

"Kutoa huduma bora kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari kupitia Ajira, Upandishwaji Vyeo na Kukuza Maadili."

"Mwalimu ni Chimbuko la Kada zote ndani na nje ya Utumishi wa Umma, hivyo anapaswa kuheshimi-wa, kujiheshimu na kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu."

MAWASILIANO:
Wasiliana na Katibu Msaidizi katika Wilaya yako au Tume Makao Makuu kupitia:-

KATIBU,
Ofisi ya Rais,
Tume ya Utumishi wa Walimu,
Mtaa wa Mtendeni,
S. L. P 353,
DODOMA - TANZANIA.

Simu: +255(26) 2322402-4
Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz
Tovuti: www.tsc.go.tz
Ukurasa wa FB: Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania,
Instagram: tumeyautumishiwawalimu
YouTube: TSC Digital Tv

# VILIO NA SIMANZI BADO VYAIANDAMA TSC, WAMLILIA JOHN SAMWEL SHIMO



*Marehemu John Samwel Shimo wakati wa uhai wake.*



*Watumishi wa TSC wakiongozwa na Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Zachary Dida (wa kwanza kulia) wakiweka shada la maua kwenye kaburi la marehemu John Samweli Shimo katika mazishi yaliyofanyika hivi karibuni wilayani Sengerema mkoani Mwanza.*

**Na Mwandishi Wetu – Dar es Salaam.**

Julai 16, 2022 inakuwa ni siku nyingine mbaya kwa watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambapo wakiwa katika mazishi ya mtumishi mwezao, Paul Salama Lekule aliyekuwa mtumishi wa Tume hiyo Wilaya ya Kongwa, zinaibuka taarifa za kifo cha mtumishi mwingine, ndugu John Samwel Shimo, Afisa Utumishi katika Ofisi ya TSC Wilaya ya Temeke.

Taarifa zaidi zilieleza kuwa ndugu Shimo alikuwa akipatiwa matibabu jijini Dar es Salaam huku akiendelea kufanya kazi katika ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Temeke.

Taarifa za Kifo cha ndugu, John Samweli Shimo zimeendelea kuwaacha watumishi wa TSC katika majonzi makubwa ikizingatiwa kuwa kwa siku za hivi karibuni kumetokea vifo kadhaa vya watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu na Wilayani.

Mbali na John Samwel Shimon na Paul Salama Lekule, watumishi wengine wa TSC waliofariki kwa siku za hivi karibuni ni Benard Nyoni, James Kalogi, Joyce Kabobo, Fredrick Kipinga, Christian Clavery, Blasio Chibupa na Yohana Peter Mpande.

# VILIO NA SIMANZI BADO VYAIANDAMA TSC, WAMLILIA JOHN SAMWEL SHIMO

Watumishi wa TSC watamkumbuka Shimo kwa uchapa kazi wake hodari, ucheshi, heshima na moyo wa kujitoa kwa kila aliyehitaji huduma na msaada wake kitu kilichomfanya kuwa rafiki wa kila mtu katika maisha yake ya utumishi kwenye ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu.

Marehemu John Samwel Shimo alizaliwa tarehe 12.12.1978 Kijiji cha Isole Wilaya ya Sengerema Mkoa wa Mwanza akiwa mtoto wa tano (5) kati ya Watoto 14 wa Bwana na Bibi. Samwel Shimo na alipata elimu yake ya msingi katika Shule ya msingi Isole iliyopo Sengerema mwaka 1984 na kuhitimu mwaka 1990.

Mwaka 1991 alijiunga na elimu ya Sekondari kidato cha kwanza, Shule ya Sekondari Kaunda na kuhitimu kidato cha nne mwaka 1994 na mwaka 1999 hadi 2000 alijiunga na Chuo Cha Jeshi la Polisi (CCP - Moshi) ambapo alimaliza na kuajiriwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kupangiwa kufanya kazi katika Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) Mkoani Dar Es Salaam.

Mwaka 2003 alijiunga na masomo ya elimu ya kidato cha sita katika kituo cha Al- Haramain Sekondari na kuhitimu mwaka 2005. Mwaka 2006 hadi 2009 alijiunga na Chuo Cha Ustawi wa Jamii Kijitonyama Mkoani Dar Es Salaam na kutunikiwa Stashahada ya Juu katika Usimamizi wa Rasilimaliwatu. Mwaka 2018 hadi 2020 alijiunga na Chuo Kikuu cha Mzumbe Tawi la Dar Es Salaam na kutunikiwa Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Rasilimaliwatu.

Kwa upande wa ajira, mwaka 2010 aliajiriwa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma (PSC) kwa cheo cha Afisa Utumishi Daraja la II na kupangiwa kufanya kazi katika Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD) Makao Makuu.

Mwaka 2016 Marehemu alihamishiwa katika Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Walimu mkoani Dodoma ambapo aliendelea kutekeleza majukumu mpaka ilipofika mwaka 2020, alipohamishiwa Ofisi ya Tume Wilaya ya Temeke ili kumuwezesha kuendelea na matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Ocen Road.

Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuzingatia Kanuni za Utumishi wa Umma ilitoa huduma zote muhimu kwa ajili kuwezesha shughuli za mazishi ya Marehemu John Samwel Shimo kufanyika kwa heshima kama mtumishi wa Umma.

Shughuli za kuaga mwili wa Marehemu John Samweli Shimo zilifanyika nyumbani kwake Dar es Salaama na baadae mwili ulisafirishwa hadi wilayani Sengerema mkoani Mwanza kwa ajili ya mazishi ambayo yalihudhuriwa na watu mbalimbali wakiwemo watumishi wa TSC.





*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Zachary Dida (wa tatu kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya watumishi wa TSC mara baada ya mazishi ya Marehemu John Samweli Shimo yaliyofanyika wilayani Sengerema mkoani Mwanza hivi karibuni.*

# TSC YATOA ZAWADI HOSPITALI YA MKOA DODOMA




*Zawadi mbalimbali zikiwa tayari kuwasilishwa Hospotali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya akinamama waliojifungua.*

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imetoa zawadi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma katika Wodi ya Wazazi ikiwa ni sehemeu ya kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Juni 16 – 23, 2022.

Miongoni mwa zawadi hizo zilizowasilishwa hospitalini hapo hivi karibuni ni sabuni, mafuta ya kupaka na taulo za watoto ambazo zililenga kuwasaidia akina mama/ wazazi katika hospitali hiyo.

Itakumbukwa kuwa TSC imekuwa na utaratibu wa kutoa msaada katika kuadhimisha wiki ya utumishi wa umma ambao mara ya mwisho watumishi wa Tume hiyo walipata fursa ya kutembelea moja ya vitoa vinavyolea watoto yatima jijini Dodoma.

Maadhimisho ya mwaka huu yalibeba kaulimbiu isemayo nafasi ya nne ya mapinduzi ya viwanda katika masuala mapya yanayojitokeza kuhusu utoaji wa huduma na urejeshwaji wakati na baadaya ya janga la Corona.

Mbali na kutembelea Hospitali hiyo, TSC iltenga sehemu maalumu ofisini hapo ambapo wateja walifika na kupatiwa huduma mbalimbali zikiwemo zinazohusiana na rufaa za walimu, upandishaji vyeo, taarifa za kiutumishi kwa ajili ya maandalizi ya kustaafu (history sheet), kupokea malalamiko na kubadilishiwa cheo/kazi baada ya kujiendeleza kimasomo.

Vilevile baadhi ya Ofisi za TSC ngazi ya Wilaya ziliadhimisha wiki ya utumishi wa umma kwa kufanya ziara shuleni nakupata fursa ya kuzungumza na walimu juu ya masuala ya Ajira, Maadili pamoja na maendeleo yao kiutumishi.



*Baadhi ya Watumishi wa TSC wakiwa tayari kupeleka zawadi kwenye Hospotali ya Rufaa ya Mkaoa wa Dodoma.*








*Watumishi wa TSC Makao Makuu, Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu, Mectildis Kapinga (kulia) na Afisa Tawala Mkuu, Omar Ilyas wakibadilishana mawazo katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma hivi karibuni.*

# WAZIRI WA ELIMU WA AFRIKA KUSINI AWAPONGEZA WALIMU KWA KUFANIKIWA UTOAJI WA ELIMU JUMUISHI NDANI YA DARASA MOJA

**Na Mwandishi wetu – Kibaha.**

Waziri wa Elimu ya Msingi kutoka Afrika Kusini Matsie Angelina Motshekga amewapongeza walimu wa Shule ya Msingi Uhuru Mchanganyiko jijini Dar Es Salaam kwa kufanikiwa katika utoaji wa elimu jumuishi kwa kuweza kuwa na wanafunzi wote katika darasa moja wakiwemo wale wenye mahitaji maalumu na kushiriki ujifunzaji katika darasa moja.

Pongezi hizo zilitolewa wakati wa ziara yake katika Shule hiyo iliyofanyika Julai 5, 2022 jijini Dar es Salaam ili kujionea uendeshaji wa mfumo wa utoaji Mafunzo Jumuishi katika ngazi ya elimu ya msingi.

Akiwa shuleni hapo Waziri huyo amefurahishwa na namna shule hiyo inavyoweza kutoa elimu jumuishi kwa kuweza kuwa na wanafunzi wote na kushiriki ujifunzaji katika darasa moja.

Aidha, Waziri Motshekga alisema changamoto kubwa iliyopo nchini mwao ni kutokuwa na mfumo jumuishi jambo ambalo linapelekea wazazi kuona watoto wenye mahitaji maalumu wananyanyapaliwa.

“Nimefurahi sana kuona namna mfumo wa elimu jumuishi unavyoendeshwa katika shule hii, nimepata funzo kubwa sana hapa ambalo tunakwenda nalo, kwetu kwani tumekuwa tukiwatenga watoto wenye mahitaji maalumu na kuonekana tunawanyanyapaa.” Alisema Waziri huyo

> ***Changamoto kubwa iliyopo nchini mwao ni kutokuwa na mfumo jumuishi jambo ambalo linapelekea wazazikuonawatotowenyemahitaji maalumu wananyanyapaliwa”.***

Kwa upande wake Naibu Waziri kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. David Silinde, alisema pamoja na Waziri huyo wa Afrika Kusini kujifunza namna elimu Jumuishi inavyoendeshwa, pia Tanzania inajifunza namna nchi hiyo ilivyofanikiwa kuifanya lugha ya alama kuwa ya lazima katika ngazi zote za elimu.

Naibu Waziri Silinde alisema anaichukua hiyo na wataijadili na viongozi wengine wa elimu kuona namna Serikali inavyoweza kuifanya lugha ya alama kufundishwa nchini kwa wanafunzi wa ngazi zote.

# PROF. MKENDA AWATAKA WATANZANIA KUTUMIA LUGHA YA KISWAHILI KWA UFASAHA ILI KUENZI UTAMADUNI WETU



**Na. Mwandishi Wetu – Dar Es Salaam.**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema watanzania lazima waenzi na kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha.

Waziri Prof. Mkenda aliyasema hayo Julai 5, 2022 jijini Dar es Salaam alipokuwa Mgeni Rasmi katika Mdahalo kuhusu Lugha ya Kiswahili na Elimu ambayo ilikua ni sehemu ya kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani iliyofanyika Julai 7, 2022.

“Roho ya nchi ni utamaduni wake, sisi Watanzania ni lazima tuwe mstari wa mbele kuhakikisha tunaongea Kiswahili fasaha, hili ni jukumu letu. BAKITA na BAKIZA muwe mstari wa mbele ili kukuza na kuendeleza matumizi ya Kiswahili na istilahi za Kiswahili.” Alisema Prof. Mkenda

Katika kuhakikisha Kiswahili fasaha kinatumika, Prof. Mkenda alisema Wizara yake itaendelea kushirikiana na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Barazala Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) katika kusukuma mbele masuala ya filamu ili kusaidia kukuza na kueneza Kiswahili ndani na nje ya nchi.

Waziri Prof. Mkenda alitumia fursa hiyo kuhimiza uandishi wa mashairi, riwaya, tamthilia pamoja na hadithi ili kusaidia kukuza lugha ya Kiswahili.

“Angalieni fursa za Kiswahili nje ya Tanzania, ukisoma Kiswahili, ni ‘dili’ na kitakupeleka ng’ambo, tunahitaji walimu wenye ufasaha katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza na uwezo mzuri wa kufundisha.” Alisema Prof. Mkenda

Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani hapa nchini kilifanyika Julai 7, 2022 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam ambapo dunia nzima ilisherehekea siku hiyo kwa mara ya kwanza baada ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kutangaza rasmi Julai 7 ya kila mwaka kuwa Siku ya Kiswahili duniani.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Bw. Saidi Yakubu alisema kuwa Serikali imeelekeza Balozi zote za Tanzania ulimwenguni kuhakikisha zinaadhimisha Siku ya Kiswahili Duniani inayofanyika kila Julai 07, 2022.

“Tumeelekeza Balozi zetu zote kote ulimwenguni kuhakikisha tarehe kila tarehe 07, 2022 wanaadhimisha Siku ya Kiswahili, siku hiyo tunataka Dunia itambue lugha hiyo kuwa Chimbuko lake ni Tanzania. Tunaamini Balozi hizo zitasaidia kutangaza vyema lugha hiyo na kutoa fursa kwa Watanzania katika kupata ajira ya kufundisha lugha hiyo Duniani.” Amesema Bw. Yakubu.

Aliongeza kuwa, Tanzania pia ilipata fursa kushiriki katika maadhimisho hayo nchini Ufaransa ambayo ni Makao Makuu ya Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) ambapo iliwakilishwa na baadhi ya Mawaziri pamoja na Msanii Mrisho Mpoto.

# TANZANIA NA AFRIKA KUSINI ZASAINI HATI YA MAKUBALIANO YA USHIRIKIANO KATIKA MAMBO MBALIMBALI YA ELIMU YA MSINGI IKIWEMO KUFUNDISHA KISWAHILI

**Na. Mwandishi Wetu – Dar Es Salaam.**

Serikali imesema itaongeza nguvu kazi, miundombinu na bajeti kwa taasisi na vyuo vinavyofundisha kiswahili ili viendelee kuandaa wataalam zaidi watakaotumika Duniani kote.

Akizungumza katika Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani yaliyofanyika jijimi Dar es Salaam kwa njia ya simu Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema Serikali itaendelea kutoa nyenzo na mafunzo ya kisasa kwa wakalimani, waandishi wa vitabu, wafundishaji wa Kiswahili kwa wageni.

Katika Maadhimisho hayo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Elimu ya Msingi ya Jamhuri ya Afrika Kusini zilitia saini Hati ya Makubaliano ya ushirikiano katika mambo mbalimbali ya Elimu ya Msingi ikiwemo kufundisha Kiswahili.

Utiwaji wa saini ulifanyika mbele ya Mhe. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda kwa upande Tanzania, na kwa Jamhuri ya Afrika Kusini ulifanywa na Waziri wa Elimu ya Msingi Matsie Angelina Motshekga.

Akiongea kabla ya utiaji wa saini Prof. Mkenda alisema baada ya kukamilika kwa maandalizi ya Hati hiyo Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliagiza kutiwa saini rasmi makubaliano hayo siku ya Kiswahili Duniani.

“Kazi ya kuandaa makubaliano haya ilifanyika kwa muda ikiongozwa na viongozi mbalimbali ambapo baada ya kukamilika Rais alituagiza tusaini makubaliano haya leo katika siku hii muhimu kwa nchi yetu.” Alisema Pro. Mkenda.

Naye Matsie Angelina Motshekga, Waziri wa Elimu ya Msingi wa Afrika Kusini alisema lengo la kusaini hati hiyo ni kufundisha Kiswahili katika Shule za Msingi na Vyuo pamoja na kukisambaza nchi nzima ili kuwawezesha Waafrika Kusini waweze kuitumia lugha ya Kiswahili.

Motshekga aliongeza kuwa kwa Afrika Kusini Kiswahili ni zaidi ya lugha kwani ni muhimu sana kwani kitasaidia kuunganisha watu wake na Bara la Afrika ambapo Kiswahili kinaongewa zaidi.

“Kiswahili kwa Afrika Kusini kitaunganisha watu wa Tanzania na kwetu pamoja na kuimarisha mahusiano ya muda mrefu yaliyopo kati ya nchi hizi mbili, na ni lazima tuhakikishe lugha hii inaunganisha watu wetu hususani vijana.” Alieleza Waziri huyo wa Afrika Kusini.





**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania